# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**KENYA HIGH SCHOOL SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# KENYA HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/1**

**KARATASI YA 1**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. Hii ni insha ya dayolojia. (Mazungumzo yanahusiana watu wawili au zaidi)

**Muundo**

a) Kichwa - Kitaje wahusika, wapi na mada.
b) Utangulizi - Kudokeza mazingira ya dayolojia kwa kifupi na maelezo yawe katika mabano
c) Mwendelezo - Mtindo wa kitamthilia utumiwe
d) Mwisho - Uamuzi kuhusu mada ujitokeze pamoja na hitimisho rasmi ya dayolojia.

- Majina ya wahusika yawepo na yaandikwe upande wa mkono wa kushoto
- Majina hayo yafuatwe na nukta pacha.
- Ufafanuzi wa matendo ya wahusika uwe kwenye mabano
- Msemaji mmoja asitawale dayolojia

**Hoja**

- Kuhamasisha wanachi kuwajibikia usalama wao.
- Kuimarisha taasisi za mahakama na jela.
- Polisi kuimarisha doria
- Kuhimiza kukubali mpango wa usalama wa nyumba kumi
- Kupiga vita ufisadi katika kikosi cha askari na washikadau katika nyanja ya usalama.
- Kuimarisha uchumi na nafasi za kazi
- Kutumia teknolojia ya kisasa kupambana na uhalifu.
- Kuongeza idadi ya walinda usalama.
- Kuwapa waalinda usalama mafunzo zaidi

–

**TAZ:** Hoja ziwe na uhalisia

Asipojikita kwenye muundo wa dayolojia aondolewe alama ($4^1/_2$) za sura

Mtahini ahakiki hoja zingine

**Swala la 2**

Ni swali la kuonyesha ukweli wa kauli aliyopewa mtahiniwa

**Hoja**

- Katiba mpya imewatengea wanawake viti na kumwacha mwanamume
- Alama za kuingia vyuo vikuu huwapendelea wasichana
- Mashirika mengi yamebuniwa kuwadhamini watoto wa kike.
- Sheria mpya za urithi zinawapendelea wanawake
- Sheria za talaka na ulezi wa watoto humpendelea mwanamke
- Hazina ya mkopo imetengewa wanawake pekee ili kujiboresha.
- Wasichana katika shule wanafadhihiwa kwa mfano kupewa visondo ilihali wavulana wametelekezwa
- Wanaume wanaodhulumu wanawake wanapata adhabu kali kisheria kuliko wanawake wanaowadhulumu wanaume.

Taz: - Mtahiniwa afanue hoja zaidi ya tano
- Zikipungua, amepungukiwa kimaudhui
- Mtahini ahakiki ufaafu wa hoja zingine

**Swali la 3**

- Hili ni swali la methali
- Maana ya juu ni kuwa anayegonga ukuta kwa ngumi anajiumiza ama kujijeruhi mwenyewe.
- Maana ya ndani ni kuwa yeyote anayeshindana na anayemzidi nguvu au uwezo huenda akajiumiza mwenyewe

**Taz:** -Mtahiniwa anaweza kuanza kwa kueleza maana ya methali kisha atunge kisa au visa

- Anaweza kutunga kisa au visa moja kwa moja ili maana ijitokeze.

- Maudhui yadhihirike kwa kuangazia pande zote mbili, la sivyo atakuwa amepungukiwa kimaudhui.

**Swali la 4**
Hili swali la mdokezo

- Mtahiniwa atoe kisa cha kusisimua kinachoanza kwa maneno aliyopewa

- Mtahiniwa atakuwa amepotoka kimaudhui kisa chake kitakapokosa kuambatana na dondoo.

- Akikosa kuanza kwa kauli aliyopewa na kisa chake kioane na kauli ataadhibiwa kimtindo tu.

- Kisa kisipooana kabisa atakuwa amejitungia swali